TOLEO LA 01

Jarida la Ni Magufuli Tena

2020 -2025

ALIAHIDI | AMETEKELEZA | APEWE TENA MITANO | AGOSTI 2020

TUMETEKELEZA KWA KISHINDO TUNASONGA MBELE PAMOJA

CHAMA CHA MAPINDUZI

MIAKA MITANO TENA KWA MAGUFULI KUZALISHA AJIRA MILIONI NANE

Mgombea wa Chama cha Mapinduzi (CCM) nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Rais, Dkt John Pombe Magufuli amesema kuwa atazalisha ajira milioni nane katika kipindi cha miaka mitano ijayo.
Rais Magufuli ametoa ahadi hiyo leo Agosti 29, 2020 Jijini Dodoma wakati wa uzinduzi wa kampeni za Chama hicho kuekea uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28 mwaka huu.

Amesema kuwa ajira hizo zitatokana na miradi mbalimbali mikubwa na kimkakati inayoendelea kutekelezwa na ile itakayotekelezwa katika miaka mitano mingine kama ikiwemo miradi ya ujenzi wa uwanja wa ndege wa Msalato, ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu pamoja na ajira za moja kwa moja kutoka Serikalini.

Aidha, Rais Magufuli amesema kuwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo Serikali ya Chama cha Mapinduzi itaendelea kusimamia amani, umoja, mshikamano, kuulinda Muungano na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar hali itakayowezesha kufikiwa kwa malengo tuliyojiwekea ikiwemo kukuza uchumi wetu kwa asilimia nane kwa mwaka," alisisitiza Dkt. Magufuli.

Akifafanua Dkt. Magufuli amesema kuwa kipaumbele kitawekwa katika sekta za kilimo, mifugo, uvuvi, miundombinu na nyingine zitakazochangia katika kukuza uchumi na kutoa ajira kwa wingi.

Aliongeza kuwa Benki ya Kilimo itaimarishwa, kuongeza eneo la umwagiliaji, kuimarisha huduma za ugani, kuboresha sekta ya uvuvi, kununua meli ya uvuvi bahari kuu.

Kwa upande wa utalii amesema wataongeza watalii hadi kufikia milioni tano, kupanua wigo wa utalii kwa kuongeza maeneo ya utalii na pia kuweka mkazo katika sekta ya Sanaa, Utamaduni, Michezo, kwa kuwa zinakua kwa kasi na zinatoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi.

Uzinduzi wa Kampeni za Chama cha Mapinduzi umefanyika leo Agosti 29, Jijini Dodoma na kuongozwa na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Rais Dkt. John Pombe Magufuli na kushirikisha maelfu ya wananchi wa Dodoma na Mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na Visiwani.

“ASANTENI WATANZANIA” - SAMIA SULUHU HASSAN

MGOMBEA Mwenza wa Urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Samia Suluhu Hassan amewashukuru watanzania kwa kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Tano katika safari ya mapambano ya vita ya kiuchumi na kujikomboa kutoka kwenye lindi la umasikini.

Samia ametoa shukrani hizo wakati wa hotuba yake fupi aliyoitoa wakati CCM, uliofanyika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma na kuhudhiriwa na viongozi wakuu wa sasa na wastaafu pamoja namaelfu ya wananchi wa Dodoma na mikoa ya jirani.

"Tunamshukuru Mungu kwa kutuwezesha kufanya tuliyoyafanya. Haikuwa safari rahisi. Nawashukuru watanzania wote kwa ushirikiano waliotupa, nawashukuru wana CCM. tulizopewa na Mungu ndizo zitakazojenga Tanzania. Sisi Awamu ya Tano tumezitumia, tumeweza kutekeleza kwa kishidno Ilani ya CCM, kwa pamoja tusonge mbele.

"Napigia mstari neno kwa pamoja. Tutasonga mbele tukifanya kampeni kwa heshima, amani na utulivu. Yote ambayo hatujamaliza yamo ndani ya Ilani ya Awamu ijayo," alisema Samia.

"ZANZIBAR TUNASUBIRI SIKU YA KUPIGA KURA TUKAMALIZE KAZI" - DKT. SHEIN

Rais wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohamedi Shein amesema wananchi wa Zanzibar wanaisubiri kwa hamu siku ya kupiga kura ili wakamalize kazi ya kuwachagua wagombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuongoza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Rais Dkt. Shein ameyasema hayo alipokuwa akimtambulisha mgombea Urais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dkt. Hussein Mwinyi katika uzinduzi wa kampeni za mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya CCM, Rais Dkt. John Pombe Magufuli na mgombea mwenza, Samia Suluhu Hassan, uliofanyika leo katika Uwanja wa Jamhuri Jijini Dodoma.

Alisema wananchi wa Zanzibarwameishaamua, wanachosubiri ni siku ya kupiga kura tu, Oktoba 28 mwaka huu ili wakawachague wagombea wa CCM kuanzia wa Serikali ya Muungano na wale wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Alisema uamuzi huo wa wananchi wa Zanzibar unatokana na sifa walizonazo wagombea wa CCM ambazo ndiyo msingi wa kuteuliwa kwao kupeperusha bendera ya chama hicho.

Akizungumza kuhusu Dk. Mwinyi, alisema ana sifa zote za kuwa Rais wa Zanzibar na anaheshimika ndani na nje ya mipaka ya Tanzania kutokana na uchapakazi wake, uadilifu na uzalendo kwa taifa. v"Mwinyi ana sifa zote za kuwa Rais wa Zanzibar, ndiyo maana amechaguliwa na CCM agombee.

Ana uwezo mkubwa, ni msomi mzuri, Daktari bingwa wa maradhi ya binadamu. Anaheshimika ndani na nje ya nchi.

"Ni mzalendo, kazi zote alizopewa na Serikali alizifanya kwa ufanisi mkubwa, mimi naamini kama ninyi kuwa atatuvusha katika uchaguzi huu.

Watu wa Zanzibar wanasubiri wakati ufike wamchague DkT. Mwinyi na sisi tulioko Zanzibar tutahakikisha anashinda," alisema DkT. Shein.

DKT. MWINYI AWATAKA WATANZANIA WASIBWETEKE, WAKAPIGE KURA

Mgombea urais wa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi kwa upande wa Zanzibar kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM), Dkt. Hussein Mwinyi amewataka watanzania wenye sifa na waliojiandikisha kupiga kura kutobweteka wakiamini kuwa wagombea wanaowataka watashinda na badala yake wajitokeze kwa wingi kupiga kura ili wawawezeshe kushinda.

Dkt. Mwinyi ameyasema hayo leo alipokuwa akiwasalimia maelfu wa wananchi waliokuwa wamefurika katika uzinduzi wa kampeni za mgombea urais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli na mgombea mwenza, Mhe. Samia Suluhu Hassan katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

"Tusimbwete, siku ya uchaguzi tukapige kura. Hili nawaomba ingawa leo siyo siku yangu nimetambulishwa tu lakini naomba niwaletee salamu za wana CCM Zanzibar kuwa wapo tayari kwa uchaguzi. Watachagua CCM.

Wanasubiri siku ya uchaguzi tu," alisema Dkt. Mwinyi.

Aidha, Dkt. Mwinyi alitumia nafasi hiyo kumshukuru Rais wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohamedi Shein kwa kufanya kazi nzuri ya utekelezaji wa ilani ya CCM ya mwaka 2010 – 2025 ambayo imekirahishia Chama hicho kazi ya kurudi kwa wananchi kuomba tena ridhaa ya kuendelea kushika dola.

Aliahidi kuendeleza kazi zitakazoachwa na Dkt. Shein na kushirikiana na Rais Dkt. Magufuli katika vita vya kiuchumi ambayo ina maadui wengi wa ndani na nje.

"Naahidi nitafanya kazi ya kuendeleza alipoachia Rais Shein kule Zanzibar, amefanya kazi nzuri, nitaiendeleza. Sina shaka na bara kutokana na kazi nzuri zilizofanyika na Rais Magufuli, akipewa miaka mingine mitano mafanikio yatakayofikiwa yatakuwa makubwa sana.

"Muhimu tuilinde amani yetu, vipo viashiria vya kuvunja amani vinavyotolewa na baadhi ya watu. Tusikubali," alisema Dkt. Mwinyi.



DKT. BASHIRU: TUMEWASHA MITAMBO YA USHINDI KWA KISHINDO

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) leo kimetangaza kuwasha mitambo yake ya ushindi katika Uchaguzi Mkuu wa Rrais, Wabunge na Madiwani.

Tangazo hilo limetolewa na Katibu Mkuu wa CCM, Dkt. Bashiru Ali alipokuwa akizungumza katika uzinduzi wa kampeni wa mgombea Urais wa CCM, Rais Dkt. John Pombe Magufuli katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Alisema CCM imewasha rasmi mitambo ya ushindi huku kikiwa na hazina ya Wabungge 18 wanaosuibiri kuapishwa tu na Madiwani katika kata zisizopungua 400 nchi nzima.

Aidha, Dkt. Bashiru alionya wale wote watakaocheza na mitambo hiyo kwani watababuka.

DKT. BASHIRU: CCM KUENZI MUUNGANO, MAPINDUZI MATUKUFU YA ZANZIBAR

CHAMA cha Mapinduzi kimesema kitaendelea kuhakikisha kuwa Tanzania inaendelea kulinda uhuru, kudumisha Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar na kuimarisha Muungano.

Hayo yameelezwa na Katibu Mkuu wa Chama hicho Dkt. Bashiru Ali wakati wa uzinduzi rasmi wa Kampeni za Chama hicho leo Agosti 29, 2020 Jijini Dodoma.
"CCM inaamini kwamba uzalendo kwa nchi ndio msingi wa maendeleo ya ukweli ya Tanzania ambayo yataletwa na watanzania wenyewe, hivyo basi, CCM itaendelea kuhimiza wananchi kuwa wazalendo kwa nchi yetu kwa kufanya kazi kwa uadilifu, bidii na maarifa kama msingi imara wa maendeleo," alisisitiza Dkt. Bashiru.
Amesisitiza kuwa CCM inaamini kuwa kila mtu ana jukumu la kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili kujiletea maenndeleo yake na Taifa kwa ujumla.

Ameongeza kuwa CCM inatambua kuwa Serikali inazoziongoza zina jukumu la msingi la kuhakikisha kuwa walio wanyonge katika jamii wanapata fursa ya kipekee ya kustawisha maisha yao na kuondokana na unyonge wao ili kupunguza tofauti za matabaka.

"CCM inatambua kuwa nchi yetu ina watu wenye uwezo na rasilimali za kutosha kama vile ardhi, madini, gesi asili, misitu, wanyama, malikale, bahari, maziwa na mito, pamoja na nafasi na fursa nzuri kijiografia", Alisisitiza Dkt. Bashiru
Alieleza kuwa rasilimali na fursa hizi zikitumiwa vizuri zitakuwa chachu kubwa kwa maendeleo ya Taifa kama ambavyo imethibitika katika utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2015- 2020.

Uzinduzi wa Kampeni za Chama cha Mapinduzi umefanyika leo Agosti 29, 2020 Jijini Dodoma na kuwashirikisha maelfu ya wananchi wa Dodoma na mikoa mbalimbali hapa nchini.

VIJANA WAMTAKA TENA MAGUFULI 2020

Wakati Chama cha Mapinduzi kikizindua kwa kishindo kampeni za Urais, Ubunge na Udiwani kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu jijini Dodoma, vijana wamewaomba watanzania watanzania kumchagua tena Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuwa ameonesha dhamira ya dhati ya kuiletea maendeleo Tanzania.

Wito huo umetolewa na vijana waliohudhuria uzinduzi kameni za CCM Jijini Dodoma ambapo wamesema kuwa katika miaka mitano ya uongozi wake, Rais Magufuli amefanya kazi kubwa ya kuijenga nchi na kueleta maendeleo.

"Nampenda Sana Magufuli, napenda pia apite kwa awamu hyingine kwa sababu ametundea mengi. Kwa miaka hii mitano tu ametenda mengi, je, tukimuongezea miaka ijayo utakuwa kuna mambo mengi zaidi," anaeleza Lulu Alex, kijana kutoka Mkoa wa Iringa ambaye alifika jijini Dodoma kushuhudia wa kampeni za CCM.

Lulu amewasisitiza vijana hasa wanafunzi kumchagua Magufuli kwani katika miaka mitano ya Urais wake amefanya mambo mengi ya maendeleo hususan maboresho katika sekta ya elimu ambapo kwa sasa wanafunzi wanasoma bila kuwa na vikwazo vyovyote.

Naye Atanas Majebele mkazi wa Dodoma amesema yeye na vijana wenzake ambao wamehudhuria uzinduzi wa kampeni za CCM wameguswa na kazi alizofanya Rais Magufuli katika kipindi cha miaka mitano hivyo wana kila sababu ya kumuunga mkono Magufuli katika kampeni za kuwania Urais.

"Tupo hapa kwa ajili ya kutoa support (kuunga mkono) lakini pia kumsikiliza mgombea ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapiduzi.

CCM ni ushindi, CCM ni Chama kikubwa na sisi kama vijana tupo pamoja usiku na mchana kuhakikisha CCM inapata ushindi," anaeleza Atanas.

"Magufuli nampa nafasi kubwa sana, amekuwa jembe sana...kama ameweza kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo kama mradi wa umeme kwa wanafunzi hawezi kutuacha.

Tunategemea makubwa kutoka kwake na ushindi," anaeleza Marko Kivamba, Mwanafunzi wa Chuo cha Mipango Dodoma.

Mwanafunzi mwingine wa Chuo hicho, Rashid Jumaanamuelezea Rais Magufuli kama ni mtu anayefanya mambo kwa vitendo. "Nafsi yangu itanisuta sana kama sitakuwa mmoja ya watu ambao wataenda kuhamasisha na kuwaambia watanzania nini Rais Magufuli amefanya na hivyo wana kila sababu ya kumchaguatena," alisisitiza mwanafunzi Marko.

CCM imezindua rasmi kampeni za Urais, Ubunge na Udiwani katika Uwanja wa Jamhuri Jijini Dodoma na kuhudhuriwa na maelfu ya wakazi wa Dodoma na mikoa jirani. Viongozi wengne waliohudhuria uzinduzi huo ni pamoja na Marais wastaafu Mzee Ali Hassan Mwinyi na Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na viongozi wengine waandamizi wa CCM.

Aidha, uzinduzi huo ulisindikizwa na burudani kutoka kwa wasanii mbalimbali wakiwemo Nassib Abdul maarufukama Diamond Platnumz, Ali Kiba, Harmonize, Barnaba Classic. Mroisho Mpoto, Mau Sama, Becker Flavour, Nandy, Chidi Benz, Banana Zoro, Weusi, SHeta, Bendi ya TOT, Hamza Kalala pamoja na wasanii wa Bongo Movie.

DODOMA YAZIZIMA UZINDUZI KAMPENI ZA CCM

Uzinduzi rasmi wa kampeni za Chama cha Mapinduzi (CCM) katika uchaguzi mkuu wa uliofanyika Agosti 29,2020 Jijini Dodoma umeifanya Tanzania na mataifa mbalimbali kuzizima kwa zaidi ya saa nane kushuhudia uzinduzi wa aina yake wa kampeni uliopambwa kwa nderemo, shamrashamra na burudani kutoka kwa wasanii maarufu nchini.

Macho na masikio ya watanzania na dunia vilielekezwa jijini Dodoma sio tu kwa ajili ya kushuhudia aina ya uzinduzi uliovunja rekodi, lakini pia kusikiliza utekelezaji wa ahadi uliofanywa na CCM chini ya uongozi wa Rais Dkt. John Pombe Magufuli pamoja ahadi zilizopo katika ilani ya Chama hicho zitakazotekelezwa katika kipindi kingine cha miaka mitano (Mwaka 2020-2025).

Kwa hakika unaweza kusema kuwa wananchi walipania kwenda kumuona Rais Magufuli ambae amekuwa na mvuto wa kipekee kisiasa yana kufanya Uwanja wa

Mbali na umati mkubwa wa wananchi kufika uwanjani, huko mitaani wafanyabiashara nao walionekana wakifuatilia kwa makini uzinduzi huo kupitia Televisheni mbalimbali zilizokuwa zikirusha mubashara uzinduzi huo wa aina yake ulifanyika Makao Makuu ya nchi.

Mabango mbalimbali yenye ujumbe wa kumpongeza Rais Magufuli, wafanyabishara kusimamisha biashara zao kwa muda kushuhudia uzinduzi, bodaboda, bajaj, mamam lishe na kila mwananchi wa Jiji la Dodoma kusimama kushuhudia uzinduzi wa kampeni za CCM kwa kufika uwanjani na pia kupitia vyombo mbalimbali vya habari ni ishara tosha kwamba Rais Magufuli amegusa maisha ya watu na anastahili kuiongoza Tanzania kwa miaka mingine mitano.

DIAMOND, HARMONIZE NA ALI KIBA WASAFISHA NJIA RAIS DKT. MAGUFULI

SHANGWE, vifijo na nderemo leo vimetawala uzinduzi wa kampeni za mgombea Urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Dk. John Pombe Magufuli na mgombea mwenza, Samia Suluhu Hassan baada ya wasanii maarufu nchini Diamond, Harmonize na Ali Kiba kualikwa jukwaani kutumbuiza kabla hajaanza kuhutubia.

Katibu wa Itikati na Uenezi wa CCM, Hamphery Polepole alimwalika kwanza mwanamuziki Harmonize kuanza kulisafisha jukwaa kwa kuwatumbuiza maelfu ya watanzania waliokuwa wamejaa pomoni katika uwanja wa Jamhuri kwa wimbo wake unaotamba sasa na unaopendwa zaidi wa watanzania wa rika mbalimbali wa 'I Wish Ningemuona Magufuli'.

Wimbo huo uliounyanyua uwanja mzima kucheza ulihitimishwa kwa sala maalumu ya kumuombea Rais Mstaafu

wa Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin Mkapa aliyefariki dunia mwezi uliopita na kuzikwa kijijini Lupaso.

Harmonize alifuatiwa na Ali Kiba ambaye aliuchezesha umati uliokuwa umefurika uwanja hapo miondoko ya muzuki wake wa 'Magufuli ni Vitendo' na aliyehitimisha ni mwanamuziki Diamond kwa wimbo wake wa 'Magufuli Baba Lao.'

Mbwembwe na mikogo ya Diamond na hasa aina yake ya kushambulia jukwaa huku akiwaimbisha mashabiki wake, ziliibua msisimkona shangwe za kumkaribishakuhutubia, Rais Magufuli ambaye baada ya kumaliza hotuba yake naye aliualika umati uliokuwa ukimsikiliza akiomba kura na kunadi Ilani ya CCM ya mwaka 2020-2025 na kuwamba wasanii wengine kuendelea kutoa burudani na kusherehekea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano.

Baadhi ya wasanii wengine waliotumbuiza ni Barnaba Classic, Shilole, Maua Sama, Backer Flavour, Lava Lava, Chid Benz, Nandy, Magufuli Gang, Bend ya TOT, Hamza Kala na wengine wengi wakiwemo wasanii wa vichekezho Joti na Masanja Mkandamizaji pamoja na wasanii wa Bongo Movie.

SOUNDTECHNIQ

BAADHI YA MASUALA ALIYOSEMA MGOMBEA WACHAMA CHA MAPINDUZI NA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA DKT. JOHN POMBE MAGUFULI WAKATI WA UZINDUZI WA KAMPENI ZA CHAMA HICHO JIJINI DODOMA AGOSTI 29, 2020

- **Ajira milioni 8 zitazalishwa katika kipindi cha miaka 5 ijayo ikiwa ni moja ya hatua za kukuza uchumi na kupunguza umasikini.**
- **Mkazo utawekwa katika mapambano dhidi ya rushwa, ufisadi na wizi.**
- **Moja ya ahadi za kipaumbele zitakazotekelezwa ni ujenzi wa uwanja mkubwa na wakisasa wa michezo hapa Dodoma.**
- **Kuongeza idadi ya watalii hadi kufikia milioni 5 ifikapo mwaka 2025, kukuza utalii wa fukwe, kuendelea kutangaza zaidi vivutio vilivyopo pamoja na kuhuisha vipindi vya chaneli ya utalii.**
- **Mapato ya sekta ya utalii yataongezeka kutoka dola bilioni 2.6 hadi dola bilioni 6.**
- **Tukuza na kuimarisha miundombinu itakayowezesha meli za utalii kuja kwa wingi hapa nchini.**
- **Tutakuza zaidi sekta ya Sanaa na Michezo, kuhuisha mfuko wa Utamaduni, kuimarisha usimamizi na hati miliki ili ziendelee kuwanufaisha zaidi wasanii.**
- **Sekta ya Sanaa na Michezo itapewa msukumo mkubwa katika kipindi cha miaka 5 ijayo.**
- **Tutaweka mjazo katika Ujenzi wa miundombinu ya barabara kuunganisha mikoa. Pia ujenzi wa madaraja likiwemo la Wami na Kigongo Busisi.**
- **Tutakamilisha upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Mtwara na ile ya Kalemii. Ni moja ya vipaumbele katika kipindi cha miaka mitano ijayo.**
- **Tutanunua Meli ya mizigo katika Bahari ya hindi.**
- **Tutajenga Meli ya kubeba mabehewa ya treni katika Ziwa Victoria na nyingine zitajengwa katika Ziwa Tanganyika.**
- **Tutanunua Ndege Tano zingine ikiwemo ya mizigo.**
- **Wasanii watapewa mikopo na kujengewa uwezo ili kuongeza tija.**
- **Megawati 5000 za umeme zitaongezwa kwenye gridi ya Taifa katika kipindi cha miaka mitano ijayo.**

- **Vijiji 9,570 vimefikishiwa umeme na Vijiji 2,680 vilivyobaki vitafikishiwa huduma ya umeme katika kipindi cha miaka mitano ijayo hivyo kufanya Vijiji vyote kuwa na umeme.**

- **Tutaendeleza ujenzi wa miundombinu ya huduma muhimu kama za afya, elimu na maji.**

- **Ujenzi wa vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya na Zahanati utaendelea katika kipindi cha miaka mitano ijayo.**

- **Ujenzi wa Hospitali za Wilaya 99, Rufaa katika mikoa 10 na za Kanda 4 utakamilishwa.**

- **Huduma za Kibingwa za afya na ubingwa bobezi zitaimarishwa hapa nchini.**

- **Watumishi wa kada mbalimbali za Afya wataongezwa kufikia 25,000.**

- **Upatikanaji wa dawa, vifaa tiba, vitendanishi utaendelea kuimarishwa.**

- **Asilimia 90 ya wananchi watafikishiwa huduma ya maji safi na salama katika kipindi cha miaka mitano ijayo.**

- **Mkazo utawekwa katika kuimarisha huduma za matibabu ya asili kwa kuwatambua na kuwawezesha watoa huduma husika.**

- **Serikali itasomesha wataalamu zaidi kupitia vyuo vya ndani na nje.**

- **Mkazo utawekwa katika kuimarisha mifumo ya utoaji haki katika ngazi zote nchini.**

Wachimbaji wadogo wataendelea kuwezeshwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

YERERE AGOSTI
CHAMA CHA MAPINDUZI

TUMETEKELEZA KWA KISHINDO TUNASONGA MBELE PAMOJA

CHAMA CHA MAPINDUZI